



TAARIFA KWA UMMA

MWENENDO WA UGONJWA WA CORONA (COVID-19) NCHINI

Dar es Salaam, Ijumaa Aprili 10, 2020

Wizara inatoa taarifa juu ya uwepo wa wagonjwa wapya **watano (5)** wa Corona (COVID-19) ambao wote ni Watanzania na ni wakazi wa Dar Es Salaam kama ifuatavyo:

1. Mwanaume mwenye umri wa miaka 68;
2. Mwanaume mwenye umri wa miaka 54;
3. Mwanaume mwenye umri wa miaka 57;
4. Mwanaume mwenye umri wa miaka 41; na
5. Mwanamke mwenye umri wa miaka 35.

Aidha, leo Waziri wa Afya wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ametangaza uwepo wa wagonjwa wapya **wawili (2)** waliothibitika kuwa na Corona (COVID-19). Hivyo sasa, jumla ya watu waliothibitishwa kupata maambukizi ya COVID-19 nchini ni **32**. Kati ya hawa **watano (5)** wamepona na wagonjwa wengine **24** wanaendelea vizuri na matibabu.

Pia, tunasikitika kutoa taarifa ya **vifo viwili (2)** vilivyotokea leo miongoni mwa wagonjwa waliothibitishwa kuwa na maambukizi ya Corona (COVID-19) nchini ambavyo ni vya;

1. Mwanaume mwenye umri wa miaka 51 Mtanzania mkazi wa Dar es Salaam tuliyemtolea taarifa tarehe 08/04/2020; na mwingine ni
2. Mwanaume mwenye umri wa miaka 57 Mtanzania mkazi wa Dar es Salaam tuliyemtolea taarifa hapo juu.

Hivyo kufanya idadi ya vifo kufikia **vitatu (3)** tangu ugonjwa huu uliporipotiwa nchini.

Kwa mara nyingine Serikali inaendelea kuwasisitiza wananchi kuchukua tahadhari ya kujikinga na ugonjwa huu kama tunavyowapatia taarifa na elimu mara kwa mara kupitia njia mbali mbali.

Umyy Mwalimu (Mb)

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO**